**MTIHANI WA MWIGO**
**MWONGOZO WA KARATASI YA PILI**

## A. SEHEMU YA KWANZA: FASIHI (ALAMA 45)

**MASWALI**

1. a) **Lipe shairi hili kichwa**
   - Siku njema itafika
   - Mwisho wa dhuluma

   **NB: Tanbihi – Kadiria majibu ya mwanafunzi**

**(1 x1 = alama 1)**

b) **Taja mambo matano anayotarajia yafike siku moja duniani**

- Fanaka kupatikana
- Haki ikatendwa na waovu kuangamia
- Uhuru wa kweli kupatikana
- Kustawi kwa mwanadamu.
- Dhuluma itakoma.
- Shida zitaondoka
- Watu watakuwa na nia moja.
- Tabu itaisha.
- Kizazi kipya kuleta usawa

**(zozote 5 x 1 = alama 5)**

c) Huku ukitaja mifano, eleza uhuru wa kishairi aliotumia mwandishi

- Tabdila mf. Balaa badala ya balia, Myake badala ya miaka.
- Inkisari

  Utapodumu – utakapodumu

  Tasitawi – Atasitawi

  Meshatwambia – ameshatwambia

  Kungia – kuingia
- Kuboronga sarufi
- Hizi shida taondoka – shida hizi
- Hili jambo – jambo hili

**(kutaja 1, mfano 1)**

**Kutaja 3 x 1 = 3**

**Mfano 3 x 1 = 3**

d) **Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi**.

i) **Balia** – shida, tabu

ii) **Matulubu** – mafanikio

iii) **Yatasibu** – yatafika, yatatimia

2. a) **Fafanua sifa za wakati kwa mujibu wa shairi**

- Huwa kam johari inayoleta bahati
- Huwa kama idhabati au ushuhuda wa baadaye
- Huleta raha.
- Hupamba medheri (mazingira) k.v makuti n.k
- Huletwa na Mungu, hukadiriwa na Mungu
- Hukoma, hufika mwisho.
- Humfanyi fukara kuwa wa kuheshimiwa.
- Wakati ni kuogopwa
- Wakati hufika mwisho

**(zozote 6 x 1 = alama 6)**

b) **Ni nini dhamira ya msanii katika shairi hili?**

- Tuwe waangalifu katika matumizi ya wakati

**(1 x 2 = alama 2)**

c) **Taja na utolee mifano tamathali tatu za usemi zilizotumiwa katika shairi hili**.

i) Jazanda

- Titila nyati
- Wakati chumo
- Wakati johari njema
- Ukienda kwa magoti
- Sitiani

- Wakati ni chuma.

ii) Tashhisi

- Wakati ni wa kusema
- Wakati hukamuliwa kwa sheke
- Raha hupamba makuti
- (wakati) ukayatema matiti

iii) Takriri

- Wakati titi la nyati kukamilika kwa shaka
- Wakati

iv) Tashbihi

- Wakati kama mnyama
- Uanguke kama mti

**(zozote 3 x 1 = 3 marks)**

d) Shairi hili ni la bahari kadha. Zitaje na uzitolee mifano.

- Manthawi – wakati johari njema, hasa ule ni bahati
- Tarbia – mishroro mine kila ubeti
- Mtiririko – neno wakati limerudiwarudiwa

**(zozote 4 x 1 = alama 4)**

## TAMTHILIA

3. i) "**Lakini ni dua za kuku ….**"

a) **Eleza muktadha wa dondoo hili.**

(i) Msemaji ni kauleni
(ii) Anajibu swali la Ngwese
(iii) Walikuwa nyumbani mwa Ngwese
(iv) Ni baada y Ngwese kuchaguliwa kiongozi w pango mara nyingine.
(v) Kauleni na Ngoi wamekija kwa Ngwese kumpongeza kwa ushindi.

**(zozote 4 x 1 = alama 4)**

b) **Taja tamathali moja ya usemi iliyotumiwa katika dondoo hili**

Methali – Dua la kuku halimpati mwewe au mdokezi – kuku ….

**(1 x 1 = alama 1)**

ii) **" Suala la ujenzi wa Jamii mpya limeshughulikiwa katika tamthilia ya Pango" Fafanua**

**kwa kutoa mifano mitano**

a) Wanawake kuheshimiwa, katango kusema huu ni wakati mwingine si wakati wa kuolewa na kupigwa na mume
b) Jamii isiyo na usaliti kama inavyojitokeza katika shairi la katando "sauti ya kizazi kipya uk 14".
c) Jamii itakayowashirikisha wanawake katika siasa na uongozi. Katango ana wania uongozi
d) Jamii ambapo vijana wataongoza si wazee. Katango ni kijana anayetaka kuongoza.
e) Jamii ambapo vijana wataheshimiwa kwa mchango wao (hadithi ya Katango ya sungura uk 42 – 45)
f) Jamii ya usawa kati ya wanaume na wanwake Katango anang'ang'ania usawa anapowania uongozi.
g) Jamii isiyo na ufisadi / kurina asali
h) Jamii isiyo na ubinafsi – Ngwese kuzingira kisima na seng'enge.

**(zozote 5 x 2 = alama 10)**

## Kithaka wa Mberia: Natali

4. a) **Watoto katika Tamthilia ya Natala wamepewa haki mbalimbali. Thibitisha kwa kutoa mifano mitano**

(i) Kupewa usalama / kulindwa na ndio sababu Natala anapoenda ufuoni kuleta mwili anawacha kina alike na bwana chini ya ulizi wa Gane.
(ii) Mapenzi – Natala anawapenda wanawe
(iii) Kupewa ushauri – Natala anawashauri wanawe kutotumia vyakula vya sukari.
(iv) Kuruhusiwa kucheza – Natala anaruhusu watoto wake kwenda kucheza.
(v) Kutendewa usawa – Tango anaporejea ananunua vobofu viwili na vinyago viwili ili watoto wapate kimoja kimoja.
(vi) Kupewa chakula – Gane anawalisha Alika na Bwanu.
(vii) Kuvishwa nguo – Natala anapiga nguo pasi
(viii) Kuandaliwa sherehe na kufurahia pamoja na wenzao – Gane anapoandaa sherehe anawaita watoto.
(ix) Kuelimishwa kwa kupewa nafasi ya kusoma – Alika na Bwanu wanapelekwa shuleni kusoma.

**(zozote 5 x 2 = alama 10)**

b) **Baadhi ya wahusika katika Tamthilia ya Natala wamefanya kazi ya wajumbe. Toa mifano mitano na ujumbe walioupeleka**

(i) Mama mwala kuleta barua na kupokeza watoto, kina Alika na Bwanu, ailikuwa, na habari kutoka kwa Tango kwamba angefika baada ya siku saba.
(ii) Chifu analetea Natala ujumbe kutoka makao makuu ya polisi, mji wa Ruma kwamba Tango alikuwa amefariki.
(iii) Mama Lime kuleta ujumbe kutoka kwa wazee wakimtaka Natala kurithiwa.
(iv) Mzee Balu kumtahamisha kasisi kuwa waendelee na sherehe za mazishi baada ya kuongea na chifu.
(v) Bala kumfahamisha familia yam zee Balu kuwa Jamaa wa Natala "shangazi" asingeweza kufika mazishini kwa kukosa nafuu.
(vi) Kasisi kuwafahamisha waombolezaji kwamba jeneza lisingefunguliwa kwa ombi la Natala.

**(zozote 5 x 1 = alama 5)**

## RIWAYA

5. **LAMIN H. OMAR: Dunia Mashaka Makuu**

**" Msiba wa Dunia ulikuwa wa kujitakia". Jadili**

- Kuiabika mbele ya pazia kunasababishwa na wepesi wake wa kudanganyika.
- Dunia anajitenga na familia kwa kwenda mjini.
- Dunia anashikwa kwa kuiba kwa hiari wakiwa na mpoto.
- Matatizo yake ya mjini yanasababishwa na kutoroka kwake nyumbani k.r kuibiwa na baadaye kufungwa kwa kupatikana akiwa uchi.
- Umaskini wake ilisababishwa na kukataa masomo
- Anakosa radhi ya baba (awali) kwa kutoroka.
- Kupuuza ushauri wa askari jela.
- Kutumia dawa za kulevya (mwasi)
- Dunia anakatwa kwa kisu na mahabusu mwenzake kwa kumwambia hatampa chakula.

Baadhi ya matatizo hakujitafutia / hakujisababishia.

- Ku7toroka kwake kunachochewa na ukali wa baba.
- Siye aliyesababbisha ajali iliyoandamnana na kuzaliwa kwake.
- Baba hakumpenda – alimpuuza.
- Baba hakumlipia karo.
- Kufa kwa dadake – Yasibu kulisababishwa na kosa la Yasibu mwenyewe.
- Inabidi kuwatunza wapwa zake na kupanga kuwarudisha nyumbani kibao ni baada ya Yasibu kufariki n.k
- Ugonjwa wa Yasibu – kumtafutia matibabu
- Hakukusudia kumuua ndama / kivunja mbuzi pembe.

**Pande zote mbili ziangaziwe**
**Kujisababishia – 8 x 1 =8**
**Kusababishiwa – 7 x 1 = 7**
**Jumla = alama 15**

6. **J. Habwe: Maisha Kitendawili**.

a) "**Mui huwa Mwema".**

**Kwa kurejelea mhusika Farida, thibitisha kauli hii.**

- Farida aliwadharau vijana akiwa chuoni.
- Hakutia bidii masomoni
- Alishiriki ulevi
- Alijihusisha na ukahaba.
- Hakuwadhamini waliomlea / msitiri mf. mjombake
- Alikuwa na majivuno.

Baadaye

- Alikuwa mfanyikazi mwenye bidii mf. Alikuwa na kampuni
- Mke mwema wa Juma
- Alimdhamini dadake kasu
- Aliwajali wafanyikazi wake mf. Mary, Juliet.

- Jirani mwema – alimsaidia bwanake Julia kuutafuta mwili wa Julia ufuoni
- Mwenye huruma na mshauri – alimshauri Rose awe na tahadhari maishani

**(zozote 12 x 1 = alama 12)**

b) Eleza jinsi maombi ya mwombaji wa Dini ya Msalaba Mweusi yalivyomfaa Farida

- Maombi yalimfaa Farida kwa:
- Alimambiwa angeanzisha kampuni yake na ikawa hivyo baadaye.
- Angekuwa mwandishi jambo ambalo lilitimia kwa kuandika kitabu.
- Alimtabiria mchangaiko yako ya kutafuta kazi yangeisha na baadaye ikawa hivyo.

**(zozote 3 x 1 = alama 3)**

## MBINU ZA KUFUNDISHIA

7. Eleza dhima ya kutumia mchezo wa kuigiza katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili

- Huimarisha lugha
- Hukuza uelewaji wa wanafunzi
- Huimarisha kumbukizi ya wanafunzi
- Hujumuisha mbinu zaidi ya moja ya kufundisha
- Huimarisha ukakamavu wa wanfunzi
- Huimarisha maingiliano ya somo moja na linguine.
- Hukuza ushirikiano baina ya wanafunzi
- Hushirikisha wanafunzi kikamilifu
- Huleta uhalisia katika somo
- Huburudisha wanafunzi
- Huimarisha matarushi
- Hukuza ubunifu wa wanafunzi
- Huteka makini ya wanafunzi
- Hukuza stadi ya kusikiliza na kuongea
- Hukuza vipawa vya wanafunzi

**(zozote 9 x 2 = alama 18)**

8. **Fafanua jinsi unaweza kufanikisha ziara ya kielimu katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili**

- Chagua mahali pa kuzuru
- Mjulishe mwalimu mkuu
- Andika barua kuomba ruhusa ya kutembelea mahali hapo.
- Julishe wazazi/ wafadhili wa watoto.
- Tembelea mahali hapo kabla ya siku yenyewe.
- Wagawe wanafunzi katika makundi na kuwapa majukumu mbali mbali
- Chagua viongozi wa vikundi
- Panga mipango ya usafiri
- Wapatie wanafunzi maagizo
- Ongoza majadiliano baada ya ziara kuhusu yaliyojiri ziarani.
- Wanafunzi waandike ripoti kuhusu ziara
- Andika barua ya shukrani.
- Wanafunzi waandike insha kuhusu ziara
- Sahihishainsha za wanafunzi
- Toa ripoti kwa mwalimu mkuu.
- Andaa walimu utaondama nao safarini
- Panga mipango mwafaka ya malazi kama wanafunzi wata lala.

**(zozote 15 x 1 = alama 15)**

9. **Vipengele vya Insha**

- Mvundo wa Insha
- Anwani / kichwa cha insha
- Utangulizi
- Mwili wa insha
- Sura ya insha
- Matimizi ya sarufi
- Uakifishaji
- Miundo ya sentensi
- Maudhui ya insha
- Matumizi ya msamiati
- Matumizi ya tamathali za usemi
- Hijai / tahajia
- Aina za insha
- Hati
- Urefu wa insha

**(zozote 14 x 1 = alama 14)**

10. **Matumizi ya 'kwa' katika darasa la saba.**

- Kuonyesha mahali
- Kuonyesha kusudi / sababu
- Kuonyesha jinsi
- Kuonyesha umilikaji
- Kuonyesha sehemu ya kitu kizima
- Hutumika katika misemo
- Kuonyesha maana ya pamoja
- Hutumika kufananisha
- Kuonyesha muda uliotumika
- Kuuliza maswali
- Kuonyesha – unganifu mf. Kula kirake

**(zozote 8 x 1 = alama 8)**